MKATABA WA KUPANGISHA KIBANDA

Mkataba huu unafanyika leo tarehe ……..

KATI YA:

NDUGU……wa S.L.P……., BABATI.

Ambayo katika mkataba huu itaitwa **(MWENYE KIBANDA)**.

NA

Ndugu, …….wa S.L.P……BABATI

Ambaye katika mkataba huu ataitwa **(MPANGAJI)**.

UTANGULIZI

a) **MWENYE KIBANDA** amekubali kumpangisha **MPANGAJI,** na **MPANGAJI** amekubali kupanga kwa ajili ya biashara KIBANDA no….. katika eneo la soko kuu iliyopo Kata ya Babati, katika wilaya ya Babati.
b) **MWENYE KIBANDA** amempangisha **MPANGAJI** kwenye Kibanda husika kwa vipindi vya miezi sita/sita hadi hapo watakapokubaliana vinginevyo.
c) Kwa kuwa **MWENYE KIBANDA** ana nia ya kupangisha na **MPANGAJI** ana nia ya kupanga Kibanda kwa malipo.

MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:

1. Kwamba **MWENYE KIBANDA** atampangisha Kibanda hicho kwa kodi ya shilingi Elfu Themanini (Tshs.80,000/) kwa Mwezi.

Kwamba mkataba huu utaanza tarehe **……../……/2017 na kuishia …../……../2017**

2. Kwamba **MPANGAJI atakuwa akilipa kodi ya** miezi 6 siku ya kusaini mkataba huu. Na atakuwa akilipa kodi zingine kabla ya tarehe 5 ya kila mwanzo wa mwezi wa kwanza wa miezi mingine 6 inayofuata.
3. Kwamba muda wa mkataba huu unaweza kuongezwa kwa upande wowote kutoa notisi ya mwezi mmoja kabla ya kumalizika muda wa upangaji.
4. Kwamba upande wowote unaweza kusitisha mkataba huu kwa kutoa taarifa ya maandishi kabla ya mwezi mmoja.
5. Kwamba iwapo **MPANGAJI** ataamua kuvunja mkataba kabla ya muda wa upangaji kuisha hatarudishiwa pesa ya kodi itakayokua imebaki kumalizia muda wa pango.
6. Kwamba iwapo **MWENYE KIBANDA** atavunja mkataba itabidi amrejeshee **MPANGAJI** kiasi cha pesa ya pango itakayokuwa imebaki kumalizia muda wa pango. .
7. Kwamba **MPANGAJI** atamruhusu **MWENYE KIBANDA / MWAKILISHI** au **WAKALA** wake kuingia kukagua matengenezo ya chumba baada ya kutoa taarifa ya kufanya hivyo. Pia **MPANGAJI** atatoa taarifa panapotokea uharibifu ili yeye aweze kufanya matengenezo.
8. Kwamba **MWENYE KIBANDA** atampangisha **MPANGAJI** kibanda kikiwa katika hali nzuri na **MPANGAJI** atamkabidhi **MWENYE KIBANDA**, kibanda kikiwa katika hali nzuri

na vifaa vyote vilivyokuwemo kabla ya upangaji baada ya kipindi cha mkataba kumalizika.

9. Kwamba **MPANGAJI** hatafanya mabadiliko yoyote kwenye KIBANDA bila kibali cha **MWENYE KIBANDA.**
10. Kwamba **MPANGAJI** atatumia kibanda alichopangishwa kwa ajili ya biashara tu na **MWENYE KIBANDA** hatambugudhi **MPANGAJI** kwa kipindi chote cha mkataba huu.
11. Kwamba **MPANGAJI** kwa namna yoyote ile hatampangishia KIBANDA hicho mtu yoyote Yule bila kibali cha **MWENYE KIBANDA.**
12. Kwamba **MPANGAJI** atahakikisha anafanya usafi wa mazingira ya ndani na nje ya kibanda na kulipia gharama zote za taka kwa mamlaka husika.
13. Kwamba iwapo **MPANGAJI** atashindwa kutimiza masharti na wajibu kama ilivyo kwenye mkataba huu na pale ambapo mkataba huu umetaja kinagaubaga, basi **MWENYE KIBANDA** ampe taarifa ya ukiukwaji huo kwa maandishi kabla ya kuchukua hatua yoyote ya kuvunja mkataba.

HIVYO KWA USHUHUDA:

Mwenye Kibanda na Mpangaji wanakubaliana kutia saini mkataba huu kama inavyoonekana hapa chini.

Mkataba umesainiwa leo hapa ……. na:

Jina :……. Leo tarehe …./…./…….}

Sahihi:……..

Ambayo katika mkataba huu ni **MWENYE KIBANDA.**

Kwa kushuhudiwa na:

Jina : ……

Sahihi: ……

Mkataba umesainiwa leo hapa Babati na:

Jina : **……** leo tarehe …./…/…...}

Sahihi: ……..
MPANGAJI

Kwa kushuhudiwa na:

Jina : ……

Sahihi: ……